# “Kipindi hiki cha corona kimekuwa kigumu”: uzoefu wa watu wenye ulemavu kuhusu gonjwa-tandavu la COVID-19 nchini Kenya

**Brigitte Rohwerder, Josephine Njungi, Mary Wickenden, Stephen Thompson, and Jackie Shaw**[1]

**May 2021**

## Muhtasari mkuu – Kiswahili Rahisi Kusoma

- Tuliwaomba watu 10 wenye ulemavu nchini Kenya watuambie kuhusu maisha yao kipindi cha gonjwa-tandavu la COVID-19. Walikuwa na aina tofauti za ulemavu kama vile ulemavu wa akili, ulemavu wa afya ya akili, ulemavu wa viungo, na ulemavu wa kutoona. Tulitaka kuongea nao kwa kuwa huwa hawaulizwi mara kwa mara kuhusu maisha yao.

### Tulichokigundua

- Janga la COVID-19 limefanya maisha kuwa magumu zaidi kwa watu wenye ulemavu pamoja na watu wengine wengi.

[1] Suggested citation: Rohwerder, B., Njungi, J., Wickenden, M., Thompson. S., & Shaw, J. (2021). ***“Kipindi hiki cha corona kimekuwa kigumu”:* uzoefu wa watu wenye ulemavu kuhusu gonjwa-tandavu la COVID-19 nchini Kenya**. Brighton: IDS, DOI: **10.19088/IF.2021.005**
Full report (in English) DOI: **10.19088/IF.2021.004**

- Ili wajikinge na COVID-19 watu waliambiwa wakae nyumbani, jambo linalofahamika kama 'lockdown'. Hii ilimaanisha watu wenye ulemavu na familia zao walipoteza kazi zao na hawakuweza kulipia chakula na dawa za kutosha. Jambo hili liliwafanya wawe na huzuni na wasiwasi sana.

- Walijikimu kwa kupewa pesa au chakula na wanafamilia wengine au marafiki, au kwa kutumia pesa waliyoweka akiba, kwa kurudi kijijini na kulima ili wapate chakula au kwa kukopa pesa. Ilikuwa vigumu kuwasaidia watu wengine kwa sababu kila mtu alikuwa na wakati mgumu.

- Baadhi ya watu pia walipata msaada mdogo kutoka kwa serikali, mashirika ya watu wenye ulemavu, au mashirika ya hisani. Lakini watu wengi hawakupata msaada wowote kutoka kwao. Kulikuwa na matatizo mengi katika usaidizi huu kwa sababu watu wengi wenye ulemavu hawakuwepo kwenye orodha ya watu waliopata fedha. Wakati mwingine pesa waliyopaswa kupewa haikuwafikia.

- Watu wenye ulemavu wa kutoona wanatumia mguso kuielewa dunia. Lakini katika kipindi cha janga la COVID-19 kugusa vitu ilikuwa si salama kwa kuwa virusi vya maambukizi vinaweza kuwa kwenye vitu. Watu hawakutaka kuwasaidia kwa njia ya kuwagusa. Hii ilimaanisha ilikuwa vigumu zaidi kwao kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kujitegemea.

- Kutoweza kukutana na watu ambao kwa kawaida huwa wanawasaidia ilikuwa jambo gumu sana kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili.

- COVID-19 imebadili jinsi kila mtu anavyoishi. Hii iliwashtua watu wengi na kuwafanya wakose uhakika kuhusu mustakabali wao

na familia zao. Kukaa nyumbani wakati wote kuliwafanya watu wakose furaha. Kutokuwa na fedha za kutosha ilisababisha migogoro katika familia. Watu waliingiwa na hofu na kupoteza matumaini – kana kwamba hakukuwa na chochote walichoweza kukifanya ili kurekebisha mambo.

- Baada ya muda ikawa salama kutoka tena nyumbani. Hii ilimaanisha baadhi ya watu walirejea kazini na kufurahi kwa sababu walipata tena pesa ya kulipia vitu kama chakula. Baadhi ya watu walikuwa na furaha kwa sababu walikuwa wamezoea jinsi mambo yalivyo sasa na hawakuwa na hofu sana.

- Lakini baadhi ya watu bado hawakuwa na kazi au pesa ya kununua chakula na bado walijawa huzuni na wasiwasi.

- Ni muhimu kwamba serikali na mashirika mengine yawasaidie watu wenye ulemavu katika kipindi cha janga la COVID-19. Wanapaswa kuwauliza watu wenye ulemavu kile wanachohitaji na namna gani msaada huu unapaswa kutolewa kwao.

## Muhtasari mkuu - Kiswahili

Gonjwa-tandavu la COVID-19 linaongeza hali iliyopo ya kukosekana usawa. Utafiti mpya unaonesha kwamba watu wenye ulemavu duniani kote wamepitia ukiukaji wa haki mbalimbali na wameathiriwa isivyo kawaida na madhara ya kiafya, kiuchumi na kijamii ya gonjwa-tandavu la COVID-19 na juhudi za kukabiliana nalo. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuangazia jinsi watu wenye ulemavu, ambao mara nyingi hawashirikishwi kwenye tafiti, walivyoguswa na mageuzi ya gonjwa-tandavu la COVID-19 nchini Kenya. Ili kuelewa vizuri jinsi gonjwa hili lililvyowaathiri watu wenye ulemavu wanaotafuta kazi, utafiti yakinifu wa kina ulifanywa nchini Kenya kama sehemu ya programu ya Inclusion Works.

**Mbinu**

Mbinu ya mahojiano ya simulizi ndiyo ilichaguliwa. Kusimulia hadithi ni njia ya asili na inayokubalika duniani kote ya mawasiliano na inawawezesha washiriki kuelezea uzoefu wao na kuweka mkazo kwenye jambo muhimu kwao. Kila mshiriki alipewa fursa ya kushiriki kwenye mahojiano mara mbili, yaliyopishana kwa miezi michache. Hii iliwawezesha washiriki kuhisi kuwa na utulivu zaidi kushirikisha uzoefu wao na kuonesha jinsi uzoefu huu ulivyobadilika kadri gonjwa-tandavu lilivyokuwa likikua. Washiriki walipatikana kwa msaada wa mashirika ya watu wenye ulemavu (OPDs) na Sightsavers. Washiriki watatu kati ya 10 walikuwa na ulemavu wa akili, watatu walikuwa na ulemavu wa afya ya akili, watatu walikuwa na ulemavu wa viungo, na mmoja alikuwa na ulemavu wa kutoona. Ili kujikinga na gonjwa-tandavu hili, mahojiano yalifanyika mtandaoni au kwa simu, na washiriki kulipiwa gharama za intaneti na usaidizi wa teknolojia. Tulikidhi pia mahitaji ya ufikio na usaidizi wa mawasiliano ya washiriki. Uchambuzi wa mada ulifanyika mtandaoni kupitia timu ya IDS na watafiti waliokuwepo nchi husika.

**Matokeo**

> “Corona imekuja na kubadilisha kila kitu.” (mwanamke mwenye ulemavu wa viungo)
>
> “Maisha yamebadilika. Hakuna pesa. Hali imekuwa ngumu.” (mwanamke mwenye ulemavu wa kutoona)

Washiriki wenye ulemavu na familia zao nchini Kenya walipitia matatizo makubwa ya kiuchumi kutokana na ‘lockdown’ na vikwazo vingine vilivyotokana na gongwa-tandavu na kuingia (zaidi) kwenye umaskini kwa kuwa wao au wale waliokuwa wakiwategemea walipoteza kazi, au kipato kingine. Wahojiwa waliripoti kupunguza ulaji wa chakula na njaa kwa kuwa hawakuweza tena kumudu milo ya kawaida, na baadhi walihofia kwamba wao na familia zao wangekufa njaa. Ongezeko la gharama za chakula na usafiri katika kipindi cha gonjwa-tandavu ilifanya mambo yawe magumu zaidi. Watu pia walihangaika kumudu gharama za kodi, dawa na mawasiliano. Janga hili la kiuchumi liliwaletea wahojiwa na familia zao mfadhaiko na shinikizo la akili kwa kuwa iliwawia vigumu kukidhi mahitaji yao.

Upotevu wa kipato na nafasi kama mkimu mkuu ilisababisha mivutano ya kifamilia, na katika baadhi ya matukio, ongezeko la ukatili wa kijinsia ulishuhudiwa kwenye jumuiya. Ili kusalimika na gonjwa-tandavu hatari zaidi na 'lockdown', wahojiwa wengi waliishi kwa usaidizi wa kifedha kutoka kwa wanafamilia wa nje na marafiki, walimaliza akiba zao au mtaji wa biashara, walikubali utaratibu wa malipo ya muda mrefu, walichukua mikopo, au walirejea vijijini ambako wangeweza kuishi kwa kutegemea kilimo. Hata hivyo, si kila mtu aliweza kuifikia mikakati hii ya kukabiliana na hali ya kiuchumi, na wanafamilia na marafiki nao pia walikuwa wakipitia magumu hayo hayo na iliwawia vigumu kusaidiana.

Watu wengi wenye ulemavu hawakupokea usaidizi wowote kutoka vyanzo vyovyote rasmi, jambo lililowasababishia madhara makubwa. Usaidizi wa usalama wa kijamii kutoka serikalini, ambao ulikuwa mchanganyiko wa programu zilizokuwepo za usalama wa kijamii na usaidizi mahsusi wa COVID-19, haukutolewa kwa watu wengi wenye ulemavu wakati wa gonjwa-tandavu hili. Matatizo ya usaidizi huu yalihusu watu wenye ulemavu kutojumuishwa kwenye orodha ya wanufaika; orodha za wanufaika kupunguzwa kwa njia ambazo hazikuwa wazi au kueleweka; pesa kutowasili wakati mwafaka; kiasi pungufu cha pesa; kutofautiana kwa kiasi cha pesa katika maeneo tofauti, pesa kwa kazi (cash for work) kutopatikana; na msaada kupelekwa kwa walezi badala ya watu wenye ulemavu wenyewe. Baadhi ya matatizo haya yalikuwepo tangu awali na baadhi yaliibuka na kupamba moto katika kipindi cha gonjwa-tandavu. Matatizo haya yamesababisha mvurugo na wasiwasi kuhusu rushwa na ubaguzi kwa watu wenye ulemavu. Matokeo yake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na hasa OPDs yalikuwa na mchango mkubwa katika kuwasaidia baadhi ya watu wenye ulemavu kukabiliana na hali. Yalitoa usaidizi wa kihisia na kivitendo. Hata hivyo, baadhi ya mashirika haya yalitapatapa kwa ukosefu wa fedha za kufanya kazi hii. Hii ilimaanisha baadhi ya watu wenye ulemavu walisikitika jinsi mashirika kwa ajili ya au ya watu wenye ulemavu yalivyofanya juhudi ndogo sana kuwasaidia wao na wengine katika kipindi hiki.

Ufikio wa huduma za afya ilikuwa tatizo kwa baadhi ya watu wenye ulemavu. Ukosefu wa vifaa vya kujikinga ilifanya baadhi ya madaktari kusita kuwatibu wagonjwa wenye ulemavu. Dawa ziliisha katika baadhi ya maeneo, na kufanya iwe vigumu kwa baadhi ya watu wenye ulemavu kupata dawa za kutibu maradhi yao. Baadhi ya kliniki zilizotumiwa na watu wenye ulemavu wa afya ya akili zilifungwa kipindi cha gonjwa-tandavu na kusababisha baadhi yao kufikwa na hali mbaya ya kiafya.

Gonjwa-tandavu hili limekuwa changamoto hasa kwa watu wenye ulemavu wa kutoona, kutokana na utegemezi wao wa kugusa, jambo linalokatazwa ili kupunguza kuenea kwa virusi. Kabla ya gonjwa-tandavu hili walikuwa wakisaidiwa na wengine, lakini hii ilikuwa ngumu sana kwa sasa kwa kuwa watu walihofia kugusana na watu wasiowajua ambao hali zao za maambukizi hazijulikani. Watu wenye ulemavu wa afya ya akili nao pia waliathiriwa hasa kwa kuwa agizo la kutokaribiana na wengine ilimaanisha hawakuweza kutegemea mitandao yao ya kawaida ya usaidizi kwa njia waliyozoea. Aidha, kuwa na ulemavu usionekana ilikuwa changamoto zaidi – ikiwa watu hao wangeshindwa kuzingatia makatazo, mamlaka zingeweza kuwa na ustahimilivu kidogo kwa makosa ya bila kukusudia. Lundo la taarifa potofu na kutishana ni mambo ambayo pia yaliwachanganya baadhi yao. Kulikuwa

pia na wasiwasi kuhusu ongezeko la unyanyasaji wa kingono kwa wanawake wenye ulemavu kipindi cha gonjwa-tandavu.

Kupotea ghafla kwa ‘ukawaida wa zamani’, mabadiliko makubwa ya maisha, na haja ya kuzoea ilimaanisha washiriki wengi walipata mshtuko na hofu kwa kuwa maisha yao ya kawaida yalivurugika kabisa. Upotevu wa uthabiti wa maisha ya kawaida uliwasababishia bumbuwazi na mashaka kuhusu mustakabali wao na familia zao, huku vikwazo vikimaanisha kwamba maisha yatakuwa ya upweke sana. Mifumo ya kawaida ya usaidizi ya watu iliathiriwa na kufanya iwe ngumu sana kwao kuzoea hali. Watu walihisi kukata tamaa, kukosa msaada, na kushuka moyo katika nyakati ngumu zaidi za janga hili. Baadhi ya watu walipata faraja katika dini na kumtumaini Mungu awapitishe salama katika hali hii.

Kadri vizuizi vilivyozidi kulegezwa na wahojiwa au familia zao kuweza kupata kazi, maisha ya baadhi ya washiriki yaliimarika kwa kuwa waliweza kukidhi baadhi ya mahitaji muhimu ya familia zao. Wengine pia walikuwa na furaha na tumaini zaidi kwa kuwa hawakuwa na hofu sana kuhusu COVID-19. Hata hivyo, wengi hawakuweza kupata kazi baada ya vizuizi kuondolewa, na bado iliwawia vigumu kuishi au kustawi. Ingawa taabu kubwa hii ilibadilika baada ya muda kwa kuwa watu walizoea hali, gonjwa-tandavu halijatokomezwa, kwa hiyo mashaka na ugumu bado unaendelea.

**Hitimisho**

Gonjwa-tandavu la COVID-19 na juhudi za serikali kukabiliana nalo ni mambo yaliyoleta athari mbaya sana na zenye madhara yaliyobadilisha maisha kwa watu wenye ulemavu, Mbinu jumuishi zinazozingatia maono ya watu wenye ulemavu kwa wakati huu wa janga kubwa lazima ziandaliwe pamoja na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa msingi wa watu wenye ulemavu unatambuliwa bila ubaguzi wa aina yoyote kwa misingi ya ulemavu.



Inclusive Futures

UKaid from the British people